

**HALMASHAURI YA WILAYA BAHU**  
**(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

Simu: +255 26 2961400  
Nukushi.: +255 26 2961401  
Barua pepe: [info@bahidc.go.tz](mailto:info@bahidc.go.tz)  
ded@bahidc.go.tz  
Tovuti: [www.bahidc.go.tz](http://www.bahidc.go.tz)



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,  
S. L. P. 2993,  
**Dodoma,**  
**TANZANIA.**

**Kumb.Na** HW/A:10/48 VOL.I/53

23 Machi, 2018

## TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi anapenda kuwatangazia Watanzania wenye sifa za kuomba nafasi za kazi ya Watendaji wa Vijiji kwa masharti ya kudumu. Tangazo hili ni baada ya kupokea kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb. Na. CFC 26/205/01 "FF" /91 cha tarehe 22/08/2017 pamoja na barua ya nyongeza ya muda wa utekelezaji wa kibali cha Ajira mbadala kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa chini ya Kumb. Na. CFC.26/205/01/ "GG"/95 cha tarehe 12/03/2018 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

### **MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 15)**

#### **Sifa za Kuingilia Moja kwa Moja:**

1. Kuajiriwa wenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu Mafunzo ya Astashahada/Cheti (NTA Level 5) katika moja ya fani zifuatazo:-
  - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **Majukumu ya Kazi:**

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, Kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora Katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa tekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati Zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu

- vi. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi Katika kuandaa na kutekeleza Mikakati ya Kuondoa njaa, umaskini na kuongeza Uzalishaji Mali.
- vii. Kiongozi wa wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika Kijiji.
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo Katika Kijiji.
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
- xii. Atawajibika kwa mtendaji wa kata.

### **Masharti ya Ajira**

Ajira ya kudumu.

### **Mshahara:**

Ngazi ya Mshahara wa Serikali **TGS B.**

### **Mambo Muhimu ya Kuzingatia kwa Waombaji:-**

- i. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania ambao hawazidi umri zaidi ya miaka 45 na hapungui umri wa miaka 18.
- ii. Waombaji wote lazima waambatanishe wasifu binafsi (CV) zenye mawasiliano ya uhakika, anuani, barua pepe na namba za simu.
- iii. Waombaji wote waombe kwa kufuata masharti ya TANGAZO LA KAZI.
- iv. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
  - a) Astashahada/cheti cha utaalamu kulingana na sifa za nafasi husika.
  - b) Cheti cha mtihani wa Kidato cha Nne au sita.
  - c) Cheti cha kuzaliwa
- v. Hati ya matokeo ya Kidato cha Nne (Result Slip) haitafanyiwa kazi.
- vi. Picha moja ya 'Passport Size' ya hivi karibuni
- vii. "Transcript" ambayo haikuambatanishwa na cheti haitafanyiwa kazi.
- viii. Kuwasilisha vyeti vya kughushi na maelezo mengine itasababisha kuchukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Waombaji ambao ni Watumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.
- x. Waombaji ambao walistaafu kazi kwasababu yoyote ile hawaruhusiwi kuomba nafasi hizi.

- xi. Waombaji waonyeshe wadhamini wawili na mawasiliano yao, anuani na namba za simu.
- xii. Waombaji wenye vyeti vya Kidato cha Nne/Sita na cheti cha Taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE).
- xiii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.
- xiv. Watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili.

**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 05/04/2018 saa tisa na nusu (9:30) Alasiri.**

Maombi yote yatumwe kwa:-  
Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Bahi,  
S.L.P 2993,  
**BAHI,**  
**DODOMA**



Daniel Kehogo

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**BAHI**

**DISTRICT EXECUTIVE DIR.**  
**BAHI DISTRICT COUN.**  
**P. O. BOX 8998**  
**DODOMA**